## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Mwaka wa 2019 Wizara ya Elimu ilizindua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kitaifa. Gredi ya 6 ndio mwaka wa 6 katika masomo ya msingi katika mtaala uliofanyiwa marekebisho. Huu ni mwanzo wa masomo ya juu katika shule za msingi kama inavyoelekezwa katika Mswada wa Bunge kuhusu Elimu ya Msingi, 2013.

Mtaala wa Gredi ya 6 uliofanyiwa marekebisho unaendeleza utekelezaji wa mtaala wa Gredi ya 3 na kijumla masomo ya Msingi kiwango cha chini. Mtaala huu unatoa nafasi kwa wanafunzi kuingiliana na mazingira yao na kukuza vipawa vyao maalum. Mbinu zinazotumiwa zinaoana na maoni na kaulimbiu ya Mtaala wa Kiumilisi kama unavyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Kuelekea kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora, faafu na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya. Mswada huu umetoa mabadiliko yanayohusisha kuvuka kutoka mtaala wa kimafunzo na kuanza kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi.

Hivyo basi mtaala wa Gredi ya 6 wa Kiswahili unalenga ukuaji wa mwanafunzi katika umilisi wa kimsingi kama: Mawasiliano na Ushirikiano, Uwazaji Kina na Utatuzi wa matatizo, Ubunifu, Uraia, Ujuzi wa Kidijitali, Hamu ya Ujifunzaji na Kujiamini pamoja na ujifunzaji wa ujuzi, stadi mbalimbali na mitazamo faafu.

Mtaala unatoa mapendekezo kwa wanafunzi kuingiliana kupitia shughuli za ujifunzaji na shughuli za kuwahusisha wanafunzi wenye uwezo tofauti wa ujifunzaji na matumizi ya mada ndogo na vipengele vingine vya Mtaala wa Kiumilisi. Matumizi ya nyenzo mbalimbali pia yamependekezwa katika mtaala huu pamoja na mbinu mbalimbali za kutathmini. Mtaala umeandaliwa kumwelekeza mwalimu kumsaidia mwanafunzi kufikia matokeo maalum yanayotarajiwa katika Gredi ya 6 na kumwandaa mwanafunzi kujiunga na Gredi ya 7 kwa utaratibu ufaao. Aidha ni matarajio yangu kuwa walimu watatumia mtaala huu kufanya ujifunzaji wa kuvutia, wa kuchangamsha na pia kuburudisha.

**DKT. BELIO KIPSANG', CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA AWALI NA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

